

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA NNE**

**11 APRILI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**KIKAO CHA NNE – TAREHE 11 APRILI, 2023**

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**39. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE  
(TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini barabara ya Manoleo hadi Kituo cha Afya Upuge itajengwa kwa kiwango cha lami.

**40. MHESHIMIWA HASAN SELEMAN MTENGA  
(MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini jengo la Manispaa ya Mtwara Mikindani litajengwa.

**41. MHESHIMIWA LUCY JOHN SABU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati wa miundombinu ya Hospitali ya Mji wa Bariadi.

**WIZARA YA KILIMO:**

**42. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na kupanda kwa bei za pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea.

**WIZARA YA NISHATI:**

**43. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Mradi wa umeme wa nguvu ya jua utaanza kutekelezwa katika Kata ya Talaga Wilayani Kishapu.

**44. MHESHIMIWA BUPE NELSON  
MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua Vituo vingi zaidi vya kuuza Gesi Asilia.

**45. MHESHIMIWA NANCY HASSAN NYALUSI  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa umeme katika Vijiji 8 vya Wilaya ya Mufindi ambavyo havijapata umeme.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**46. MHESHIMIWA ROBERT CHACHA MABOTO  
(BUNDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA katika Halmashauri ya Mji Bunda.

**47. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,  
Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni nini mpango wa Serikali katika  
kuhakikisha elimu inayotolewa inaendana na  
mahitaji ya sasa.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**48. MHESHIMIWA JOHN MARKO SALLU  
(HANDENI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na  
Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi kwa kiwango  
cha lami kipande cha barabara ya Turiani hadi  
Handeni Km 104.

**49. MHESHIMIWA KUNTI YUSUPH MAJALLA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na  
Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itamalizia kulipa fidia Wananchi  
wa Makole waliopisha upanuzi wa Uwanja wa  
Ndege na Mkonze waliopisha ujenzi wa SGR.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA  
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**50. MHESHIMIWA JANETH ELIAS  
MAHAWANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,  
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali haioni haja ya kufunga mtandao wa  
*Wi-Fi* maeneo yote nchini kufuatia jamii  
kuhamasika na matumizi ya teknolojia.

**WIZARA YA MAJI:**

**51. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya  
kukamilisha Ujenzi wa Mradi wa maji Tukuyu  
Mjini.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA  
BIASHARA:**

**52. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP  
MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji,  
Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha *Special Economic Zone* ili kuchochea viwanda vya uchakataji Njombe Mjini.

### III. HOJA ZA SERIKALI:

#### WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

*(Majadiliano yanaendelea)*

DODOMA  
11 APRILI, 2023

N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE